

## Maswali

1. Mariamu aliishi wapi?
2. Nani alikuja kuona Mariamu?
3. Malaika aliambia Mariamu nini?
4. Malaika aliambia Yusufu nini?
5. Mungu alikuwa amesema Mwanawe atazaliwa wapi?
6. Mbona Mariamu na Yusufu walienda Bethlehemu?
7. Mbona Yusufu na Mariamu walikaa kwa boma la ng'ombe?
8. Yesu alizaliwa wapi?
9. Wachungaji waliona nini?
10. Malaika aliambia wachungaji nini?

## Majibu

1. Mariamu aliishi Nazareti.
2. Malaika alikuja kumwona Mariamu.
3. Kwamba atapata mtoto, naye ni Mwana wa Mungu.
4. Kwamba mtoto mwenye Mariamu ako naye ni Mwana wa Mungu, ilibidi amuoet Mariamu.
5. Mungu alisema Mwanawe atazaliwa Bethlehemu.
6. Kaisari aliamrisha kwamba kila mtu lazima aende kwa mji wa familia yao ili watozwe kodi.
7. Hakukuwa na nafasi kwenye nyumba ya wageni.
8. Yesu alizaliwa kwa boma la ng'ombe.
9. Wachungaji waliona mwanga mkuu na malaika wengi wakimsifu Mungu.
10. Kwamba mwokozi amezaliwa Bethlehemu katika boma la ng'ombe.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1   Mwaka wa 3**



## 36 Yesu anazaliwa

### Marejeo

Luke 1: 26 – 38 na 2: 1 – 20; Mathayo 1: 18 – 25

### Kiini cha somo

Kujifunza juu ya kuzaliwa kwa Yesu Mwana wa Mungu, kusiokuwa kwa kawaida

### Maneno maalum

- 36.1 Mariamu + Nazareti + ameposwa kwa Yusufu + malaika + mtoto + Mwana wa Mungu
- 36.2 Yusufu + hofu + malaika + mtoto + Mwana wa Mungu + Yusufu na Mariamu walioana.
- 36.3 Bethlehemu + Kaisari + sheria + Yusufu na Mariamu + safari
- 36.4 Bethlehemu + Mariamu amechoka + nyumba ya wageni + hakuna nafasi + boma la ng'ombe + Mwana wa Mungu akazaliwa + hori.
- 36.5 Wachungaji + Mwanga mkuu + malaika + habari njema + Mwokozi + Bethlehemu + hori + jawa na furaha

**36.1** Wakati mmoja kulikuwa na mwanamwali, jina lake aliiitwa Mariamu. Aliishi kwa kijiji cha Nazareti. Alikuwa ameposwa kuoleka kwa Yusufu, mseremala. Lakini siku moja kitu cha ajabu kilitendeka kwa Mariamu. Alikuwa kwa shuguli zake za kawaida, punde tu aliangalia juu na akaona mgeni. Mariamu alikuwa na uoga kwa sababu yule mgeni alikuwa na uzo wa nguvu na nyororo kama wa malaika wa Mungu.

Mungu alikuwa ametuma malaika kwa Mariamu. Mariamu alikuwa na uoga. Malaika alimwambia, "Usiogope." Mariamu alitulizwa na maneno yake na akasikiliza ujumbe kutoka kwa Mungu.

Malaika alimwambia Mariamu kwamba atapata mtoto na huyo mtoto ni Mwana wa Mungu. Huyu mtoto atakuwa mkuu na Mungu atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi. Atatawala Israeli milele na Ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Malaika alipokuwa ameenda, Mariamu alibaki akitetemeka. Alikumbuka ahadi yenye Mungu alikuwa ameahadi Daudi kwamba kutakuwa na Mwanawe atakayekaa kwa kiti chake milele. Mungu alikuwa amesema, "Nitakuwa Baba yake na yeye atakuwa Mwanangu." Atakuwa mama wa Mwana wa Mungu!

**36.2** Yusufu alihofia Mariamu, lakini usiku moja alipokuwa akilala, katika ndoto zake aliona malaika. Malaika alimwambia kwamba asiogope kumuoa Mariamu. Mtoto aliyembeba ni mwana wa Mungu. Mungu alikuwa amemchagua Yusufu kulinda mtoto na mama yake. Kwa hivyo Yusufu na Mariamu walioana.

**36.3** Mungu alikuwa amenenea nabii mmoja wa Akano la Kale kwamba Mwanawe atazaliwa kule Bethlehemu. Lakini Yusufu na Mariamu waliishi Nazareti iliyokuwa mbali na Bethlehemu. Siku moja habari ilitoka kwa Kaisari ikisema eti sheria iko ya kusema kwamba kila mtu aende kwa mji wa familia yao na atozwe kodi kule. Mji wa Mariamu na Yusufu ulikuwa Bethlehemu. Muda mchache kabla ya mtoto kuzaliwa, Yusufu na Mariamu waliondoka wakasafiri mwendo mrefu kwenda Bethlehemu. Walienda mwendo mrefu kwa barabara ya vumbi. Mariamu alichoka sana, sana lakini hakulalamika.


**36.4** Mwishowe walifika Bethlehemu. Yusufu alimchukuwa Mariamu kwa vijia vya mji mpaka kwenye nyumba ya wageni. Alikuwa na wasiwasi juu ya Mariamu kwa sababu alikuwa amechoka na mtoto alikuwa karibu kuzaliwa. Alitakiwa pahali pa kupumzikia.

Walipofika kwa nyumba ya wageni, Yusufu alienda haraka kupata pahali pa kukaa. Lakini hakukuwa na nafasi hapo ndani, kwa hivyo alirudi kwa huzuni,

Mwenye nyumba ya wageni alihurumia Mariamu kwa sababu alikuwa amechoka sana. Aliita Yusufu na kumwambia kwamba wangekaa kwa boma la n'gombe pamoja na wanyama kwa usiku huo tu. Yusufu alimshukuru. Alimwongoza Mariamu katikati ya umati wa watu na wakaenda mpaka kwa boma la n'gombe. Pale alimtengezea majani ya wanyama ili apumzike kwa wanyama.

Baadaye usiku huo, Mwana wa Mungu alizaliwa. Malaika wa Mungu walifurahi. Yusufu alimchukua mtoto na akampa Mariamu. Mariamu alimfunga kwa nguo za kitoto na kumweka kwa hori la n'gombe.

**36.5** Kondeni karibu na Bethlehemu kulikuwa na wachungaji wakilinda kondoo wao. Mwanga mkuu uliwazunguka na malaika akazungumza nao. Wachungaji waliogopa. Lakini malaika aliwambia, "Msiogope. Nawaletea habari ya ajabu kutoka kwa Mungu. Mwokozi amezaliwa Bethlehemu. Yeye ni Masiya. Mtapata mtoto amefungwa nguo za kitoto na amelala horini." Punde tu kulikuwa na malaika wengi angani wakimsifu Mungu.



Baada ya malaika kuenda, wachungaji walienda Bethlehemu. Walipata Yusufu na Mariamu na mtoto aliyekuwa amelala horini. Wachungaji walijazwa na furaha na wakasifu Mungu kwa kuwaonyesha Mwanawe.